AfyaMtandao Newsletter
No. 03 - Aprili 2009

Tume ya Kikristo ya Huduma za Jamii (CSSC)

AfyaMtandao Newsletter

No. 03 - Aprili 2009

Karibu Afyamtandao!!

Bw. Petro Masatu Pamba, Mratibu Afyamtandao

Mwaka 2008, ni mwaka ambao mradi wa AfyaMtandao ulianza kutekelezwa rasmi ambapo semina na warsha mbalimbali zilifanyika na zingine zimeendelea kufanyika mwaka huu. Semina hizo ni; Mfumo wa kuhifadhi taarifa za afya kwa njia ya Kompyuta (HMIS), Tibamtandao (Telemedicine) Mwanza na Arusha, Telemedicine platform na eLearning iliyofanyika hivi karibuni Dar es Salaam.

Mtandao huu umeanzisha kundi la majadiliano linalofahamika kama AfyaMtandao Dgroup, ni kundi linalowakutanisha watumishi na wadau wa afya, waandishi wa habari ambao kwa pamoja wanajadili na kushirikishana utaalamu kuhusu mada mbalimbali zinazohusu Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEKNOHAMA) katika sekta ya afya

Ili kuweza kujiunga unakaribishwa kutembelea afyamtandao@dgroups.org na elewa kuwa AfyaMtandao inaboresha huduma ya afya kwa njia ya TEKNOHAMA.

Wasiliana na Afyamtandao:
S.L.P 9433
DAR ES SALAAM
TANZANIA
SIMU: +255 22 2112918; 2123730
MOBILE: 0755393624, 0754770866, 0784412091
BARUA PEPE: afyamtandao@afyamtandao.org
TOVUTI: www.afyamtandao.org

CSSC yazindua filamu za makala ya afya

Tume ya kikristo ya huduma za jamii (CSSC) kupitia kitengo cha AfyaMtandao kinachosimamia idara ya mawasiliano, imezindua filamu tatu ambazo zinaelezea huduma ya afya kwa njia ya TEKNOHAMA na njia ya kuwatunza watoto wanaozaliwa katika uzito mdogo ambao hawajatimiza miezi tisa ya kuzaliwa inayojulikana kama Kangaroo.

Filamu hizo ambazo baadaye zitapelekwa kwenye vituo mbalimbali vya Television hapa nchini zinahusu Tibamtandao (Telemedicine) jinsi inavyofanyakazi kwa baadhi ya hospitali za kanda ya kaskazini, Mfumo wa kuhifadhi taarifa za afya za wilaya kwa njia ya kompyuta (DHMIS) na Kangaroo Method.Filamu hizi zimeezewa kwa lugha Kiswahili lakini pia zimetafsiriwa kwa subtitles za kiingereza kwa wale ambao hawajui Kiswahili ili na wao wapate kufahamu kinachoelezewa.

CSSC, wizara ya afya, wadau na miradi mingine ya afya watatumia filamu hizo katika kuhamasisha umuhimu wa kutumia TEKNOHAMA katika sekta ya afya na kujifunza kutumia njia ya kangaroo ili kuondokana na vifo vya watoto wanaozaliwa katika umri huo mdogo.

Uzinduzi huo ulianza kwa wafanyakazi wa CSSC makao makuu kuonyeshwa filamu hizo na wao kupata nafasi ya kutoa maoni kuhusu filamu hizo ambazo zimekuwa ni kivutio kikubwa kwa wale wote waliopata nafasi ya kuzitazama.

iicd
People - ICT - Development

Wachukuaji wa picha za filamu hiyo wakiwa kazini

Kubadilishana Maarifa Miongoni mwa Wataalamu wa Afya

Matumizi ya Teknolojia Habari na Mawasiliano katika utoaji na usimamizi wa huduma ya Afya nchini Tanzania bado ni mgeni. AfyaMtandao inawaleta pamoja watoa huduma za afya,watungaji wa Sera na wadau wa Maendeleo katika kupanua wigo na kubadilishana maarifa katika maeneo mbalimbali ya Afya.Maeneo haya yanajumuisha;Tibamtandao (Kutibu wagonjwa kwa kupata maelekezo kutoka kwa madaktari wengine kwa njia ya Mtandao),Usimamizi wa utunzaji taarifa kwa njia ya mtandao (HMIS) na Masomo kwa njia ya Kompyuta au Mtandao (e-learning kwa watumishi wa Afya. AfyaMtandao inafadhiliwa na Taasisi ya kimataifa ya Mawasiliano na Mawasiliano ya nchini Uholanzi (IICD) kwa ushirikiano na Shirika la Swiss agency tangu 2006.

Kujenga jukwaa la kushirikishana uzoefu na hospitali zingine

Mikakati ya kuboresha Mawasiliano katika sekta ya Afya imeenea nchi nzima na kila aina ya hospitali ina mpango wake.Kutokuwa na umoja ikiwa na maana kuwa kutokuwa na sauti za pamoja,makubaliano ya pamoja au majadiliano ambapo mashirika na taasisi zinazotoa huduma ya Afya zinaweza kubadilishana na kujifunza uzoefu ambao watanufaika nao.

AfyaMtandao inajaribu kuziba pengo hilo kwa kujenga jukwaa la majadiliano ambapo wataalamu wa TEKNOHAMA (ICT) katika huduma ya afya wataweza kubadilishana maarifa na kuweka sera kama muongozo katika kazi. Mtandao unasimamia mahitaji kutoka kwa wanachama wake.

Wizara ya afya yatembelea mradi wa DHMIS Mwanza

Ujumbe wa watu kutoka Wizara ya Afya kwa kushirikiana na Tume ya Kikristo ya huduma za Jamii (CSSC), ulifanya ziara ya kutembelea Mradi wa kuhifadhi taarifa za afya za wilaya (DHMIS) na kujionea jinsi mfumo huo unavyofanya kazi katika kurahisisha utoaji huduma za afya kwa baadhi ya hospitali na Zahanati za mkoa Mwanza.

Ujumbe huo ulioongozwa na Mkurugenzi wa CSSC Dk.Adeline Kimambo ulitembelea Kituo cha Afya Nyakato kinachomilikiwa na Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT),Zahanati ya Makongoro na hospitali ya wilaya ya Nyamagana Butimba. Ujumbe huo uliwajumulisha Bw.Jovin Mukela mkuu wa Kitengo cha Kompyuta wizarani, Bi.Regina Kikuli Mkurugenzi wa Sera na Mipango wizara ya afya.

Wengine ni Dk.Sylivester Budeba Mwakilishi wa Kitengo cha Ushirikiano kati ya Serikali na mashirika binafsi katika wizara na Bw.Petro Pamba Ofisa kitengo cha Mawasiliano (CSSC) na Mratibu wa AfyaMtandao.

Pamoja na kutembelea sehemu hizo pia ujumbe huo ulipata nafasi ya kutembelea Halmashauri ya Jiji la Mwanza kitengo cha afya ambapo taarifa na ripoti zote za Afya zinapelekwa.

Ujumbe ulivutiwa namna mfumo huo unavyorahisisha kazi na kupunguza msongamano wa wagonjwa kwenye hospitali na vituo vya Afya kwa kurahisisha Mawasiliano ambao unatumia "Software" ya "AfyaPro" ambapo Mgonjwa anaposajiliwa taarifa zake zinahifadhiwa katika Kompyuta na hivyo kuwa rahisi kuzipata.Pia mfumo huo unasaidia kujua idadi ya wagonjwa waliosajiliwa kwa siku na udhibiti wa mapato,kujua idadi ya dawa zilizomo katika Bohari kirahisi na unasaidia katika kuandaa ripoti. Ujumbe huo umeahidi kuwasilisha taarifa hizo kwenye vikao mbalimbali vya Wizara.

Mfumo wa DHMIS kupitia "Afya-Pro" unafadhiliwa na shirika la kimataifa la Mawasiliano na Maendeleo (IICD) ambapo Afyamtandao inashiriki katika kuboresha mradi huu.

Warsha za Afyamtandao zaonyesha mafanikio

Warsha mbalimbali zilizofanywa na Afyamtandao 2008, kwa kushirikiana na Tume ya Kikristo ya huduma za jamii (CSSC) na IICD, zimeonyesha mafanikio na tayari hospitali nane zimejiunga na kuwa wanachama wa Afyamtandao.

Hospitali hizo na sehemu zilizopo kwenye mabano kuwa ni Sumve (Mwanza), Sengerema (Mwanza), Rubya (Kagera), Kagondo (Kagera), Mugana (Kagera), Biharamulo (Kagera) Bulongwa (Iringa), Kolandoto (Shinyanga), Berega (Morogoro) na Zahanati ya Ukombozi iliyoko wilaya ya Bunda.

Hospitali hizo baada ya kujiunga na kuwa wanachama zitanufaika kwa kuhudhuria mikutano yote ya TEKNOHAMA (ICT) itakayokuwa inaandaliwa na Afyamtandao, kupewa kipaumbele katika mafunzo ya (ICT)

kwa watumishi na kupata vifaa vya ICT kama vile kompyuta,printer nk. kwa gharama nafuu,faida nyingine ni kutengenezewa makala zinazohusu shughuli zao kupitia kitengo cha habari (Media) na msaada katika shughuli za ununuzi wa vifaa vya ICT. Ada ya kujiunga kuwa mwanachama wa Afyamtandao ni Tshs 50,000 na ada ya mwaka ni Tshs 120,000

eLearning kwa Maendeleo ya Sekta Afya

Tume ya Kikristu ya Huduma za Jamii (CSSC) kupitia mradi wa AfyaMtandao kwa kushirikiana na Taasisi ya Kimataifa ya Mawasiliano na Maendeleo (IICD),imefanya Warsha ya Masomo kwa njia ya TEKNOHAMA (eLearning) kwa lengo la kuboresha sekta ya Afya nchini.

Warsha hiyo ya siku moja ilifanyika katika ukumbi wa baraza la Maaskofu Katoliki Tanzania (TEC)-Kurasini Dar es salaam.

Lengo la Warsha hiyo iliyohusisha washiriki kutoka katika Taasisi za Afya nchini ilikuwa kujifunza kuhusu elearning jinsi inavyofanya kazi na kubadilishana utaalamu katika kuboresha na kuendeleza taaluma hiyo nchini Tanzania.

Katika warsha hiyo washiriki walijadili mambo muhimu ambayo yanapaswa kupewa kipao mbele ili kuzidi kuboresha huduma hiyo.Baadhi ya mambo hayo ni pamoja na kupandisha madaraja wahusika wa sekta hiyo kwenda kiwango cha juu, kuhamasisha wadau wa Afya kuhusu faida ya masomo hayo, kuainisha maeneo husika ya mafunzo,walengwa na mapato, na kuendeleza taaluma hiyo katika maeneo yote ya nchi.

Baadhi ya waratibu wa miradi walielezea miradi yao. Bw Petro Pamba Mratibu wa AfyaMtandao aliezea kuhusu AfyaMtandao jinsi inavyofanya kazi na mafanikio iliyoyapata tangu ilipoanzishwa Januari 2008, Bw.Dennis Mazali Mratibu wa eLearning alielezea mradi huo kwa washiriki jinsi unavyofanya kazi na changamoto zinazojitokeza katika mradi huo. Naye Bi. Miep Lenoir kutoka shirika la IICD linalofadhili miradi hiyo aliwasilisha jinsi ambavyo Shirika lao linavyoshiriki kikamilifu katika kuboresha huduma za Afya kwa njia ya TEKNOHAMA.

NJIA YA KANGAROO

Hospitali ya Sengerema na njia ya Kangaroo kwa watoto

Katika kuokoa vifo vya wakina mama na watoto wadogo, hospitali ya wilaya ya Sengerema iliyopo mkoani Mwanza ambayo inamilikiwa na kanisa Katoliki jimbo la Geita,imeanzisha njia rahisi ya kuwatunza watoto ambao wanazaliwa kabla ya kufikia siku zao za kuzaliwa, miezi tisa na kuwa na uzito mdogo.

Njia hiyo inayojulikana kama Kangaroo, haina gharama na haiitaji vifaa kama vile "incubator", imebuniwa kutokana na mnyama Kangaroo jinsi anavyobeba mtoto wake, imeanza kutumika hospitalini hapo tangu 1990 na imesaidia kupunguza vifo vya watoto wanaozaliwa katika umri mdogo ukilinganisha na wakati ule njia hii ilipokuwa haitumiki.

Akizungumzia jinsi njia hiyo inavyotumika Mganga Mkuu wa hospitali hiyo Sr.Dkt. Mariajose Voeten anasema kuwa njia hiyo inatumika pale mtoto ambaye hajatimiza uzito na umri unaotakiwa anapozaliwa,huwekwa katika kifua cha mama kwa kulalia tumbo na kufungwa na kitenge ili aweze kupata joto ambalo humsaidia mtoto kukua na kuongezeka uzito unaotakiwa.

Mama hutakiwa kukaa masaa 24,lakini kutokana na mahitaji yake muhimu huweza kutoka mara 4 hadi 6 kwa vipindi vya dakika 10-15 ili kuweza kula na kujiweka katika hali ya usafi.Mama hutakiwa kumnyonyesha mtoto mara kwa mara kila baada ya saa moja na nusu na kutakiwa kujitahidi kumsaidia mtoto wake ili afikie uzito wa kutosha.

Sr.Dkt.Mariajose anasema,njia hiyo ilianzishwa na Mama wa Kiholanzi Bi.Kamstra kwa kushirikiana na binti yake ambaye alikuwa anasomea uuguzi katika hospitali hiyo,imeleta mafanikio makubwa kwa kusaidia kuokoa watoto wengi wa aina hiyo ambao wamezaliwa hospitalini hapo kwa kipindi cha zaidi ya miaka 17 tangu njia hiyo ianze kutumika.

Aidha,Dkt Mariajose anasema moja ya faida kubwa ya njia kangaroo ni kwa baadhi ya wakina mama na walezi waliotumia njia hii,kuwafundisha wakina mama wengine waliopo vijijini jinsi ya kutumia njia hii.

Hospitali ya Sengerema ni hospitali teule ya wilaya ambayo inatoa huduma mbalimbali zikiwemo za wagonjwa wanaokuja kutibiwa na kuondoka,wanaolazwa,upasuaji, macho,meno nk.